**MKATABA WA UMILIKISHAJI WA SHAMBA LA UWEKEZAJI**

**(LILILOPO LUHAFWE-TANGANYIKA)**

**BAINA YA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA TANGANYIKA**
**(HALMASHAURI)**

**NA**

..................BITENDELO FARMS LIMITED..................

**(MWEKEZAJI)**

Certified true copy of the Original
Sign: [signature] Date: 25/5/2021
VERONICA VICTOR TESHA
Advocate, Notary Public & Commissioner for Oaths

**MKATABA WA MAUZIANO YA SHAMBA LILILOPO LUHAFWE, TANGANYIKA.**

**MKATABA HUU** wa mauzo ya shamba unafanywa leo tarehe ....29....mwezi..04...mwaka.2021.........

**KATI YA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA TANGANYIKA, (Taasisi ya Serikali) wa S. L. P 01, MPANDA** (ambaye katika mkataba huu atajulikana kama **Halmashauri**) kwa upande mmoja;

**NA**

~~Bwana/Bi~~/Kampuni/~~Taasisi~~......BITENDELO FARMS LIMITED......,
Mtanzania mwenye ~~kitambulisho cha kupigia kura~~/ ~~NIDA~~/TIN ~~chenye~~ Na.....145-361-532......... wa S.L.P 96 Mpanda, Katavi,ambaye atajulikana kama **Mwekezaji** kwa upande mwengine;

**KWA KUWA** Halmashauri ni mmiliki halali wa shamba lenye ukubwa wa Ekari ____500____ **na** kama itakavyoelezwa hapo chini lenye miti mchanganyiko lilichopo eneo la Luhafwe, Wilaya ya Tanganyika, Mkoa wa Katavi.

**NA KWA KUWA** Halmashauri kwa hiari yake na kwa ridhaa yake amekubali kuhamisha umiliki wa shamba lenye ukubwa wa ekari...500......na haki zote zilizopo juu yake kwa Mwekezaji kwa masharti kama yatakavyoelezwa katika mkataba huu kwa madhumuni pia kama yatakavyotajwa;

**NA KWA KUWA** Mwekezaji yuko tayari kumilikishwa shamba hilo kwa lengo la kuwekeza katika kilimo kwa mujibu wa sheria za Tanzania zinazohusu Ardhi;

**NA KWAKUWA** Halmashauri na Mwekezaji walishajadiliana vya kutosha juu ya suala hili na sasa wameamua kuweka mkataba unaoelezea kuhusu masharti ya makubaliano hayo;

**KWA HIVYO BASI MKATABA HUU UNASHUHUDIA KAMA IFUATAVYO;**

1. Kwamba Halmashauri inammilikisha Mwekezaji jumla ya ekari......500.................za nchi kavu na ekari...................za mbuga;

2. Kwamba thamani ya shamba husika ni shilingi za kitanzania (Tsh)....50,000,000.................kwa mujibu wa taarifa ya uthamini iliyofanyika mwezi octoba 2020 ambayo itadumu hadi juni 2021;

3. Kwamba malipo ya shamba hilo yanapaswa yawe yamekamilika kabla/ifikapo juni 30, 2021;

4. Kwamba umiliki wa shamba hilo utaendelea kubakia kwa Halmashauri hadi Mwekezaji atakapokamilisha malipo kwa mujibu wa mkataba huu;

5. Kwamba wale wote watakaokuwa na madai juu ya shamba hili baada ya kumilikishwa kwa Mwekezaji, basi madai yao yote wayaelekeze kwa Halmashauri na Mwekezaji hatokuwa na dhima yoyote juu ya hili na wala haki zake hazitoathiriwa na madai hayo au upungufu wowote juu ya umiliki unaotokana na ama taarifa zisizokamilika au zisizo sahihi zilizotolewa na Halmashauri;

6. Kwamba Wahusika wote wanakubaliana kwamba masharti yaliyomo humu yataendelea kuwa na nguvu za kisheria na kuwafunga kila muhusika akiwemo yeye binafsi ama wakala wake, mrithi au msimamizi wa mali;

7. Kwamba Masharti ya mkataba huu yanatawaliwa na sheria za Tanzania na hivyo yatatafsiriwa kwa mujibu wa sheria hizo.

8. Kwamba Mwekezaji akishalipa gharama stahiki kwa mujibu wa mkataba na kutimiza masharti ya umilikishwaji atatumia shamba kwa madhumuni ya uwekezaji katika kilimo na si vinginevyo;

9. Kwamba Mwekezaji anatakiwa kuanza uzalishaji katika shamba/eneo lake ndani ya muda wa miezi 24 baada ya kusaini mkataba;

10. Kwamba ikitokea Mwekezaji anataka kuhamisha umiliki kwa mwingine, masharti ya mkataba huu yataendelea kubakia baina ya Halmashauri na Mwekezaji mpya;

11. Kwamba katika hatua za awali za kusafisha shamba, Mwekezaji anatakiwa kuomba mwongozo katika ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Tanganyika ili kupata utaratibu wa uvunaji wa maliasili zilizomo shambani;

12. **Matendo yaliyo nje ya uwezo wa kibinadamu**

Hakuna upande wowote wa mkataba huu utakaofikiriwa kuwa umeshindwa kutimiza wajibu wake ikiwa utekelezaji wake umezuiliwa au kucheleweshwa kwa sababu ya vita, mapinduzi, ghasia za kiraia, magonjwa ya mlipuko, ajali, moto, mafuliko, upepo mkali, tetemeko la ardhi, au kwa sababu nyingine zozote zilizo nje uwezo wa upande ulioathirika, ikiwa notisi ya maandishi ya kutokea kwa tukio hilo na madhara yake kwa upande huo kutekeleza wajibu wake inatolewa ndani ya siku thelathini (30) toka tukio lilipotokea ambalo liko nje ya uwezo wa kibinadamu.

13. Mara baada ya tukio hilo kuisha, upande ulioathiriwa na tukio hilo utautarifu upande mwingine.Ikiwa pande zote za mkataba huu zitazuiliwa kutekeleza wajibu wake na hali ya tukio hilo linaloisha kwa muda wa zaidi ya miezi mitatu, pande za mkataba huu zitashauriana na kuamua namna ya utekelezaji wa wajibu wao kwa muda ujao. Hakuna upande wowote wa mkataba huu utakaokuwa na haki ya kudai fidia kutoka kwa upande mwingine kwa sababu ya kutokea kwa tukio lililo nje ya uwezo wa binadamu.

14. **Utatuzi wa migogoro**

Mgogoro wowote unaoweza kutokea kati ya pande za mkataba huu kuhusiana na tafsiri ya mkataba huu au kifungu chochote juu ya haki na wajibu wa kila upande utatatuliwa na pande zote kwa njia ya amani. Ikishindikana, mgogoro utatatuliwa na wasuluhishi kwa njia ya usuluhishi.

Kila upande utachagua msuluhishi mmoja na mwenyekiti atachaguliwa kwa maridhiano ya pande zote. Uamuzi utakaofikiwa na Mwenyekiti utakuwa wa mwisho na unaozibana pande zote. Hata hivyo upande wowote unaweza kufikisha mgogoro huo mahakamani bila kuufikisha kwa msuluhishi.

15. Mkataba huu unafuta makubaliano mengine yote yaliyotangulia juu ya umiliki wa sehemu ya shamba hili.

**KWA KUSHUHUDIA** basi wahusika wanaweka saini zao siku na tarehe kama ilivyotajwa hapo juu.

**KWA NIABA YA HALMASHAURI YA WILAYA YA TANGANYIKA:**

JINA Romuli R. John

SAHIHI ______________________________

WADHIFA DED - Tanganyika District Council

ANWANI S.L.P 1, Mpanda, Katavi

TAREHE______________________________

**SIMU** 0784428273

**Mbele ya:**

JINA Hamad Mapengo

SAHIHI ______________________________

WADHIFA Chairman - Tanganyika District Council

ANWANI S.L.P 1, Mpanda, Katavi

TAREHE______________________________

SIMU 0757213600

**KWA NIABA YA MWEKEZAJI:**

JINA Ng'ombe Yared Bitendelo

SAHIHI ______________________________

WADHIFA Chief Executive Officer

ANWANI S.L.P 96 Mpanda, Katavi

TAREHE______________________________

SIMU 0766226688

**Mbele ya:**

JINA Exavier Yared Bitendelo

SAHIHI ______________________________

WADHIFA Consultant

ANWANI S.L.P 96 Mpanda, Katavi

TAREHE ______________________________

SIMU 0763261874

# JEDWALI.

**SHAMBA** lote lenye miti mchanganyiko ambalo lina ukubwa wa Ekari ..........500.......... lililopo Luhafwe, Wilaya ya Tanganyika Mkoa wa Katavi lenye majira ya nukta kama ifuatavyo:

**Kaskazini:** $p_1$ WDG 554 (260372.34,9365177.92)

**Kusini** : $P_2$ WDG 560 (260800.09,9362707.26)

**Mashariki:** $P_3$ WDG 561 (261507.04,9363468.82)

**Magharibi:** $P_4$ WDG 555 (259691.77,9364444.81)

Certified true copy of the Original
Sign: ..... Date: 25/5/2021.
VERONICA VICTOR TESHA
Advocate, Notary Public & Commissioner for Oaths

# HALMASHAURI YA WILAYA YA MPANDA
(MPANDA DISTRICT COUNCIL)
## STAKABADHI YA ADA YA KAWAIDA
(GENERAL RECEIPT) **No.**

Payer ID: 307900003733

Balance: 0

**Nimepokea kutoka kwa** 10411

**Anuani** BITENDELO FARMS LIMITED

**Hesabu ya shilingi** MPANDA

**Kwa ajili ya Kodi ya** Twenty Five Million Only

**Mtaa/ Eneo** SALE OF PLOTS(2020/2021)

**Kasma** ________ **Taslimu/ Hundi Na** ________

**TShs.** 11460104 25,000,000.00

Jina la Mpokeaji: Jacqueline Christian Kayombo

Sahihi ya Mpokeaji ________ Cheo REVENUE ACCOUNTANT Tarehe 21/04/2021






Certified true copy of the Original
Sign: ________ Date: 25/5/2021
VERONICA VICTOR TESHA
Advocate, Notary Public & Commissioner for Oaths

# SHAMBA LA **BITENDELO FARMS LIMITED** ENEO LA RUHAFWE WILAYA YA TANGANYIKA MKOA WA KATAVI.




## COORDINATES REFERENCES

WDG 555= 9364444.81, 259691.77
A= 9364387.42, 259736.54
B= 9364048.32, 259952.85
C= 9363709.22, 260169.17
D= 9363375.71, 260381.92
E= 9363030.81, 260601.93

WDG 560= 9362707.26, 260800.09
F= 9362913.78, 261003.37
G= 9363139.04, 261212.44
H= 9363364.91, 261422.08

WDG 561= 9363468.82, 261507.04
I= 9363802.86, 261293.43
J= 9363802.86, 261071.91
K= 9364469.93, 260850.52
L= 9364803.36, 260629.13
M= 9365136.79, 260407.74

WDG 554= 9365177.92, 260372.34
N= 9365067.92, 260281.86
O= 9364842.10, 260072.20
P= 9364616.89, 259863.09